

JINA: ..... NAMBARI: .....

SAHIHI: ..... TAREHE: .....

SHULE: .....

102/2

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

JULAI / AGOSTI 2013

MUDA: SAA 2 ½

## MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI YA KATI 2013

CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI

KISWAHILI

LUGHA

KARATASI YA PILI

MUDA: 2 ½

### MAAGIZO

1. Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
4. Hakikisha ya kwamba maswali yote yamo na kuwa kurasa zote zimepigwa chapa kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
<b>JUMLA</b>	<b>80</b>	

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kiingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kuutawala ulimwengu wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyehobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi hujihusisha sana katika kutandaridhisha aina moja au nyingine ya amara muhimu za kitandaridhi. Hizo ni kama vile biashara za kimataifa, lugha za kimataifa, aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile pop, reggae, ragga, rap, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, san asana, lugha ya Kiingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika.

Utandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendesha maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia had nyingine wakitumia vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi vya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, hata za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme radio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa kupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la Uingereza na CNN la Marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. Hawa hawana mipaka, wote wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindaki kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta mlahaka mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imeupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, wakereketwa wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Vile vile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zinazofungamana na tamaduni hizo.

Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekana kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote, ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adau kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama chungu mbovu, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha.

- (a) (i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto.

(alama 2)

.....  
.....

- (ii) Tohoa maneno mawili kutokana na neno kutandaridhisha kisha ueleze maana ya maneno hayo.

(alama 2)

.....  
.....

- (b) Ni nini maana ya “hawa hawana mipaka.”

(alama 1)

.....

- .....
- (c) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN? (alama 2)
- .....
- .....
- (d) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao. (alama 2)
- .....
- .....
- (e) Je, watandaridhi unalumiwa kwa nini katika kifungu hiki? (alama 2)
- .....
- .....
- (f) Msemu: “Chungu mbovu” ni msemu wa kimtaani tu. Mwemo sawa ni upi? (alama 1)
- .....
- (g) Eleza maana ya: (alama 3)
- (i) Amara:.....
- .....
- (ii) Mlahaka:.....
- .....
- (iii) Wakereketwa:.....
- .....

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Maendeleo ya taifa hutegemea jinsi wananchi wanavyojitolea katika kulibingirisha gurudumu la uchumi wao. Kila mwanajamii anahitajika kujibidiisha katika kazi au taaluma yake. Mzalendo yeyote yule hupata motisha ya kufanya kazi iwapo anaweza kupata ile kazi aliyokuwa akitamani.

Kumakinika katika taaluma fulani si jambo jepesi na huchukua muda kutengeneza. Kwa mfano, ili mhazili apate staha ya uhazili sharti apatie ngazi mbali mbali. Mwanzo kabisa lazima ahitimu vyema katika masomo rasmi darasani. Masomo hayo pamoja na cheti huweza kumpa fursa ya kujiunga na vyuo mbalimbali vya uhazili. Anapojiunga na vyuo hivyo ndipo safari inapoandaliwa. Kukamilisha safari hii kunahitaji muda wa miaka minne. Anapohitimu huwa tayari ameimudu shughuli hiyo. Hata hivyo, anatakiwa afanye mazoezi kila mara ili asisahau yanayohitajika katika taaluma hiyo.

Wengi waliokwishapata ujuzi huo wa uhazili huona kuwa hawatapata kazi nzuri yenye mshahara mkubwa. Baadhi yao hujilinganisha na wale wenzao ambao katika masomo wana utaaluma kama wao. Ijapokuwa wote ni wahazili, viwango vyao ni tofauti na mishahara pia hutofautiana. Tofauti hapa ni daraja zao za vyeo. Baada ya kuhitimu na kupata vyeti vya uhazili ni rahisi kupata au kutopata kazi zenye ujira wa kuvutia. Anayefanikiwa ana safari ya kujikakamua hasa kwa upande wa uzingativu wa

kazi kikamilifu na kutunza hadhi ya ofisi yake.

Kuna mashirika makubwa yanayojweza kiuchumi, ambayo rasilmali yake ni imara. Mashirika madogo huwa yana rasilmali yanayoyumbayumba. Mashirika haya yana wahazili na wafanyikazi ambao hupata mishahara duni.

Wafanyikazi hawa hufanya kazi kwa kutokuwa na uhakika wa kulipwa mishahara mwisho wa mwezi. Watu kama hao hawawezi kutilia maanani kazi zao. Mashirika mengine hayana utaratibu maalum wa kulipa mishahara kwa vile hetegemea utu wa mkurugenzi. Baadhi ya wakuu hawa huwa na wabanizi na huwapuja wafanyikazi wao. Hili ni swala nyeti ambalo linahitaji litatuliwe kwa kuwa na chama cha kupigania haki za wafanyikazi. Wakati wanapotafuta kazi, wahazili wengi huwa ni wahitaji na hukubali chochote wanachopewa.

Wale waliobahatika kupata nafasi ya ujira katika kampuni kubwa za kimataifa, mishahara huwa ni ya kutia moyo. Katika dunia hii wahazili wana vibarua vigumu kwa sababu lazima wapate tajriba na uzoefu wa taaluma inayoendelea na shirika fulani. Wakurugenzi mara nyingi huwa hawana subira. Mhazili anapotumia msamiati usioenda sambamba na shughuli za kiofisi hawasiti kufoka. Wavumilivu miongoni mwao hula mbivu. Hawa hawafi moyo bali hujitahidi zaidi ili wasikumbwe na kimbunga cha kufokewa. Kuna wengine ambao humwaga unga.

(a) Fupisha aya ya tatu za kwanza (maneno 60 – 70)

(alama 6)

**Matayarisho**

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

**Nakala safi**

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....  
(b) Huku ukizingatia aya mbili za mwisho, eleza masuala muhimu ambayo mwandishi anaibua. (maneno 65 – 70) (alama 7)

**Matayarisho**

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

**Nakala safi**

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

.....  
3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Toa mifano miwili miwili ya sauti zifuatazo. (alama 2)

(i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo.

.....  
.....

(ii) Sauti sghuna ambazo ni vikwamizo

.....  
.....

(b) Onyesha mofimu katika: (alama 3)

Mliopewa

.....  
.....  
.....  
.....

(c) Andika sentensi hii iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Mwashigadi alimwambia shangazi yake kuwa angempokea mjomba iwapo angempata.

.....  
.....

(d) Bainisha vitenzi katika sentensi hii. (alama 3)

Amina ndiye mwizi aliyekuwa akiiba mifugo wa jirani.

.....  
.....  
.....

(e) Andika sentensi hii katika hali ya kutendwa. (alama1)

Mzee analima shambani.

.....  
.....

(f) Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mgeni aliandaliwa chakula kitamu na mwenyeji wake kwa sinia.

.....  
.....  
.....  
.....

(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 5)  
Mwanafuni aliyewachochea wenzake ni adui mkubwa mno.

(h) (i) Kishazi ni nini? (alama 1)

.....

(ii) Kwa kutumia mfano mmoja wa sentensi, onyesha aina za vishazi. (alama 2)

.....

.....

(i) (i) Kiimbo ni nini? (alama 1)

.....

(ii) Eleza matumizi ya kiimbo. (alama 2)

.....

(j) Onyesha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mtoto aliyezaliwa jana jioni akilia ametushangaza mno.

.....

.....

(k) Jibu kulingana na maagizo. (alama 2)

(i) Ufisadi (unda kitenzi)

.....

(ii) -pya (unda nomino)

.....

(l) Eleza maana mbili zinazopatikana katika sentensi hii. (alama 2)

Huyu amekuja kutuliza.

.....

.....

(m) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Aliangika bendera baada ya kifo cha mfalme wao.

.....

(n) Kanusha sentensi ifuatayo kwa umoja. (alama 1)

Sisi ndio tunaopenda kuchezea haki za watoto.

(o) Tunga sentensi ukitumia kirejeshi tamati. (alama 1)

(p) Eleza maana zinazotokana na vivumishi katika sentensi zifuatazo. (alama 3)

(i) Mwanasiasa mwenye ukabila hafai.

(ii) Kitabu kingine kitanunuliwa

(iii) Serikali yenyewe iliwatisha raia.

(q) Bainisha aina ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo: (alama 2)

(i) Wewe ulimpiga yule.

(ii) Mfupi ana vitatu.

(r) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya -a- (alama 1)

Kibofu hupaa angani.

#### 4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Huku ukitoa mifano, taja na ueleze sifa zozote **tano** za sajili ya bunge. (alama 5)

(b) Eleza sifa zozote **tano** za lugha. (alama 5)



For More Free KCSE past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

